



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA MBUNGE WA VITI MAALUM

KUPITIA CHAMA CHA MAPINDUZI

Dodoma, 4 Februari, 2021

Kufuatia kifo cha Mhe. Martha Jachi Umbulla, Chama cha Mapinduzi kilikuwa na nafasi moja (01) wazi ya Ubunge wa Viti Maalum.

Kwa mujibu wa Ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A(8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume inatakiwa kujaza nafasi wazi ya Mbunge wa Viti Maalum kwa kuzingatia orodha ya majina ya wagombea wanawake ambayo iliwasilishwa Tume na chama cha siasa kwa ajili ya uchaguzi mkuu.

Hivyo, baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume katika kikao chake cha tarehe 4 Februari, 2021 imemteua Ndg. Yustina Arcadius Rahhi kuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi.

Imetolewa na:

Dkt. Wilson Mahera Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi